BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI YA BARAZA LA WAWAKILISHI, KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA UWEKEZAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE

# YANAYOHUSIANA NA HAYO

Mheshimiwa Spika,

Naanza hotuba hii kwa kumshukuru Mola Mtukufu, aliyetujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako Tukufu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili hatimaye tuweze kuuchangia kwa umakini mswada uliopo mbele yetu kwa maslahi ya Taifa letu.

Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niwasilishe maoni ya Kamati kuhusiana na "Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo".

Mheshimiwa Spika,

Kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ujasiri wake katika jukumu zima la uongozi wa Nchi hii sambamba na jitihada anazochukua za kuendeleza sekta ya Uwekezaji na sekta nyengine hapa nchini.

Mheshimiwa Spika,

Tunatoa shukurani za dhati kwa Makamo wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa busara zake na ushauri anaompatia Mhe. Rais katika mambo mbali mbali kwa ustawi wa nchi yetu na watu wake. Kadhalika tunamshukuru Mheshimiwa Hemed kwa kusimamia vyema shughuli za Baraza hili akiwa ni kiongozi wa shughuli za Serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi, AidhaKamati yangu ya Uchumi pia inampongeza Makamo wa kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa jitihada zake anazozichukuwa katika kumsaidia kazi Mheshimiwa Rais,na juhudi zake katika kuendeleza maridhiano miongoni mwa wananchi wa Zanzibar,kwani nchi inapokosa hali ya utulivu ,shughuli za kiuchumi husimama na kupelekea uchumi wa nchi hiyo kudhooufika.

Mheshimiwa Spika,

Naomba sasa nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa nchi Afisi ya Rais Kazi,Uchumi na Uwekezaji Mheshimiwa Mudrik Ramadhan Soraga pamoja na timu yake ya watalaamu ikiongozwa na Mwanamama Mahiri Katibu mkuu wa Uwezeshaji Ndugu Khadija Khamis Rajab kwa mashirikiano yao waliyoipatia Kamati yetu katika kipindi chote cha majadiliano ya Mswada huu.

Mheshimiwa Spika,

Napenda kuwashukuru Wanasheria wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu kwenye ngazi ya Kamati.

Mheshimiwa Spika,

Kwa kuwa Mswada tunaoujadili ulileta kwako kwa hati ya dharura, na kutokana na uharaka wake,Kamati ilikosa fursa ya kuwaalikwa wadau mbalimbali ili kuujadili Mswada huo kama inavyoelekezwa na kanuni ya 84 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020.Hivyo basi, Kamati inaendelea kutoa pongezi kwa wizara ya Nchi Afisi ya Rais,Kazi,Uchumi na Uwekezaji kwa jitihada zake za kuleta wataalamu, tarehe 28 Febuari, 2022 kwa ajili ya kuwaelemisha Waheshimiwa Wajumbe dhana nzima ya kuanzisha kwa Wakala huo.

Mheshimiwa Spika,

Mafunzo yaliotolewa na Wizara yalijikita katika kufanunua Dhana nzima ya Wakala huo ikiwemo Muundo wake, Kazi zake,upatakanaji wa watumishi wake na nguvu utakaopewa Wakala huo kwa mujibu wa sheria. Pia wataalam walitoa mafunzo kuhusiana na mswada wenyewe kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika,

Natoa pongezi za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Uchumi kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuujadili na kuuchambua mswada ulioletwa mbele yao kwa upeo na ustadi wa hali ya juu. Naomba sasa niwape fursa Wajumbe wa Baraza hili kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii mmoja baada ya mwengine kama ifuatavyo:

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Juma Makungu Juma - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mjumbe
4. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
6. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Mjumbe

7. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf - Mjumbe

8. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

Mheshimiwa Spika,

Katika uchambuzi wa Mswada huu, Kamati yangu ilifanya kazi na makatibu wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia na kuturahisishia kuuchambua ipasavyo mswada huu, naomba nao niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo;

1. Ndugu Noman Thabit Noman -Katibu
2. Ndugu Asma Ali Kassim -Katibu.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yetu inaipongeza Serikali kwa kuleta mswada huu katika wakati mwafaka ambapo nchi yetu imo kwenye mageuzi ya kiuchumi kutoka uchumi wa kutegemea kilimo hadi uchumi wa viwanda. Ni matumaini yetu kuwa, uanzishwaji wa Wakala wa Uwezeshaji wananchi Kiuchumi nchini utawawezesha Wajasiriamali na wazalishaji wadogo wadogo kupiga hatua zaidi za uzalishaji na kupata masoko ya ndani na ya nje ya nchi, chini ya usimamizi wa wakala unaoanzishwa na sheria hii. Hatua hii ni muhimu sana kwani uanzishwaji wa Wakala huo utapelekea kuzalisha ajira kwa vijana na kupunguza umasikini wa kipato kwa wanachi wetu.

Mheshimiwa Spika,

Ni ukweli usiopingika kuwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu unategemea sekta ya viwanda na uvuvi kwa asilimia kubwa. Wakala huu utakapoanzishwa utakua na uwezo wa kutoa mikopo kwa ajili ya uwezeshaji kwa wajasiriamali wadogowadogo kwenye sekta tofauti za uzalishaji na kupelekea kupunguza wimbi la umasikini na kutatua kwa kiasi kikubwa tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika,

Mswada huu unaweka mazingira rafiki na wezeshi kwa wawekezaji na Wajasiriamali wa ndani ili kuwekeza kwenye sekta mbalimbali za kiuchumi. Ni dhahiri kuwa, kupita kwa mswada huu kutaifanya Zanzibar kufungua milango na fursa za kuinua uchumi wetu na kupelekea Pato la Taifa (G.D.P) kuongezeka maradufu.

Mheshimiwa Spika,

Kimsingi, Kamati yangu inakubaliana na dhana nzima iliyobebwa na mswada huu pamoja na marekebisho madogo madogo iliyoyapendekeza wakati ilipokaa na Wizara kwa ajili ya kuupitia mswada huu. Marekebisho hayo yamegawika katika sehemu mbali mbali zikiwemo makosa ya kiuandishi, makosa katika uteuzi wa maneno, makosa ya kukosekana kwa baadhi ya vitu muhimu na vya msingi kuwemo katika mswada huu.

Mheshimiwa Spika,

Kamati inapendekeza Kifungu cha 6 kifanyiwe marekebisho kama ifuatavyo:

a) kwa kufutwa aya ya (h) na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

“kuanzisha na kuendeleza Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa wa Shughuli za Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi katika sekta mbali mbali na kuwezesha usambazaji wa taarifa”.

Mheshimiwa Spika,

Kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta maneno “na weledi” na kuweka badala yake maneno “weledi na jinsia”. Kamati yangu inapendekeza marekebisho hayo ili kuzingatia uwiano wa jinsia katika usimamizi na uendeshaji wa Wakala.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inapendekeza Kifungu cha 9 kifanyiwe marekebisho katika aya (a) kwa kuongeza maneno “katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali” mwishoni mwa aya hiyo. Aidha, marekebisho kama hayo tunapendekeza yafanyike katikaaya ya (a) ya kifungu cha 17.Hii ni katika kuhakikisha kwamba tunapata Mwenyekiti mwenye sifa zinazokubalika.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inashauri kifungu cha 30 kifanyiwe marekebisho katika kifungu kidogo cha (2) kwa kuongeza maneno “itakayotolewa na Wakala” mwishoni mwa kifungu kidogo hicho ili kukamilisha maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika,

Katika sifa za kusajiliwa kwenye Wakala unaoanzishwa, Kamati yangu inapendekeza kuongeza aya mpya ya (g) baada ya aya (f) katika kifungu cha 32 na kisomeke kama ifuatavyo:

“(g) awe muadilifu wa hali ya juu”.

Mheshimiwa Spika,

Ili kuweka nidhamu kwa wajasiriamali watakaosajiliwa chini ya Wakala utakaoanzishwa, Kamati yangu inapendekeza kuongeza

kifungu kidogo kipya cha (2) katika kifungu cha 36 na kisomeke kama ifuatavyo:

“Endapo Mjasiriamali au Mfanyabiashara amefutiwa cheti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atatakiwa kulipa deni analodaiwa”.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inapendekeza kufanya marekebisho kwenye jadweli la mswada huu katika kifungu cha 9(d) kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

“(d) isipokuwa Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji, kusitishwa na Waziri kwa kushindwa kutimiza matarajio ya Wakala”.

Mheshimiwa Spika,

Marekebisho mengine yaliyofanywa na Kamati yangu yameainishwa kwenye waraka wa marekebisho ambayo tayari yameingizwa kwenye Baraza mtandao.

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika,

Mwisho niwashukuru Wajumbe wote kwa utulivu wenu na naomba tuuchangie, tuujadili, tutowe mapendekezo na hatimae tuupitishe mswada huu.

Mheshimiwa Spika,

Kwa niaba ya Kamati yangu, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………

Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar.